Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project

Published on *Books on Islam and Muslims* | *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Aya 224 -227: Yamini

Wala msimfanye Mwenyezi Mungu ni pondokeo la viapo vyenu.

Mwenyezi Mungu amekataza kutangulizwa katika kila jambo kwa kuapa sana. Kwa sababu mwenye kukitaja kitu sana amekijaalia ni pondokeo lake. Mwenyezi Mungu ameshutumu kuapa sana kwa kauli yake.

وَلَا تُطِعْ كُلَّ حَلَّافٍ مَهِينٍ {10}

“

W

ala

usimtii

kila

mwenye

kuapa

sana

aliye

dhalili."

(68:10)

Mwenye kuapa sana haiba yake hupungua, huzidi dhambi zake na atatuhu– miwa uongo.

(Ili) mfanye mema na mumche (Mwenyezi Mungu) na muwe wema kati ya watu.

Hili ndio sababu ya kukatazwa kuapa; maana yake Mwenyezi Mungu anawakataza kuapa bila ya dharura, ili muwe wema wanaomcha Mungu, wenye kufanya wema duniani na wala sio wenye kufanya ufisadi.

Mwenyezi Mungu hatawashika kwa sababu ya kuapa kwenu kwa upuzi upuzi.

Baada ya kukataza Mwenyezi Mungu kuapa bila ya dharura amebainisha kwamba mengi yanayowapitia watu katika ulimi mfano *'Wallahi vile'* au *'sio hivyo Wallahi',* n.k. hayo siyo viapo vya uhakika isipokuwa ni mchezo tu unaokuja kwenye ulimi bila ya kukusudia, wala hayana athari yoyote. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu hakuwajibisha kafara katika dunia wala hakuna adhabu katika akhera.

Lakini atawashika katika yaliyokusudiwa na nyoyo zenu.

Kwa sababu Mwenyezi Mungu Ambaye umetukuka utukufu wake, haangalii sura na kauli, bali huangalia nia na vitendo, kama anavyosema:

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ وَلَٰكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا عَقَّدْتُمُ الْأَيْمَانَ ۖ فَكَفَّارَتُهُ إِطْعَامُ عَشَرَةِ مَسَاكِينَ مِنْ أَوْسَطِ مَا تُطْعِمُونَ أَهْلِيكُمْ أَوْ كِسْوَتُهُمْ أَوْ تَحْرِيرُ رَقَبَةٍ ۖ فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ ۚ ذَٰلِكَ كَفَّارَةُ أَيْمَانِكُمْ إِذَا حَلَفْتُمْ ۚ {89}

"Mwenyezi Mungu hatawashika kwa viapo vyenu vya upuzi, lakini atawashika

kwa

viapo

mlivyoapa

kwa

nia mliyoifunga

(barabara).

Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha wastani mnachowalisha

watu

wa

majumbani

mwenu

au

kuwavisha,

au

kumwacha

huru mtumwa.

Asiyeweza

kupata hayo,

basi

afunge siku tatu. Hiyo

ndiyo kafara

ya

viapo

vyenu

mnapoapa...."

(5:89)

Mtu aliyebaleghe, mwenye akili timamu mwenye kukusudia na aliye na hiyari, akiapa na akakhalifu, basi itampasa kutoa kafara ya kumwacha huru mtumwa au kuwalisha au kuwavisha maskini kumi. Akishindwa hivyo atafunga siku tatu. Tumezungumzia zaidi kuhusu kiapo, sharti zake na hukumu zake katika juzuu ya tano ya *Fiqhul-Imam Jaffar Sadiq.*

Kwa wale ambao wanaapa kujitenga na wake zao ni kungojea miezi minne. Na kama wakirejea basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu. Na wakiamua talaka basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

Kuapa kujitenga katika sharia ni kuapa mtu kuwa hatamwingilia mkewe. Mafaqihi wa Kishia wameshartiza kuwa mke awe ameingiliwa; kama si hivyo hakitakuwa kiapo; na kuwe ni kuapa mume kuacha kumwingilia mkewe muda wa maisha yake au muda unaozidi miezi minne, kwa sababu mke anayo haki ya kuingiliwa angalau mara moja kila miezi minne kwa uchache.
Wamesema: Kama atamwingilia kabla ya miezi minne atatoa kafara na kizuizi kitaondoka; kama vile hakikuwa kitu, na ikipita zaidi ya miezi minne wala asimwingilie; kama mke akisubiri na akaridhia, hiyo ni juu yake wala haifai kwa yeyote kumpinga. Na kama akishindwa atamshtaki mume kwa hakimu wa sheria. Baada ya kupita miezi minne atalazimishwa kumrudia au kumwacha, akikataa atafungwa mpaka achague moja wapo ya mambo mawili; wala si haki kwa hakimu kumwachisha kwa nguvu. Kama mume ataamua kurudi, basi atatoa kafara iliyotajwa.

وَالْمُطَلَّقَاتُ يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ ثَلَاثَةَ قُرُوءٍ ۚ وَلَا يَحِلُّ لَهُنَّ أَنْ يَكْتُمْنَ مَا خَلَقَ اللَّهُ فِي أَرْحَامِهِنَّ إِنْ كُنَّ يُؤْمِنَّ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ وَبُعُولَتُهُنَّ أَحَقُّ بِرَدِّهِنَّ فِي ذَٰلِكَ إِنْ أَرَادُوا إِصْلَاحًا ۚ وَلَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۚ وَلِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ {228}

Na wanawake

waliopewa

talak

a

wangoj

e

tohar

a

tatu wal

a

s

i

halal

i

kwa

o

kuficha

alichokiumba Mwenyezi

Mung

u

katik

a

matumb

o

yao,

ikiwa wanamwamini

Mwenyez

i

Mung

u

n

a

Sik

u

ya

Mwisho. Na waume zao

wan

a

hak

i

zaid

i

y

a

kuwarudi

a

katik

a

mud

a

huo

,

kama

wakitaka

kufanya suluhu. Nao (wanawake) wanayo

hak

i

saw

a

n

a

il

e

iliy

o

ju

u

yao

kwa sharia. Na

wanaume wana daraja zaidi kuliko

wao

.

Mwenyez

i

Mung

u

ana nguvu

,

Mweny

e

hekima.

Source URL: https://www.al-islam.org/sw/al-kashif-juzuu-ya-pili/aya-224-227-yamini